



POSTA NA SIMU SAVINGS AND CREDIT

CO-OPERATIVE SOCIETY LIMITED

REG. No. DSR. No.118

P.O. Box 3948 Dar es Salaam Tel: 022-2182267/2182077 Fax 2182053

WARAKA WA NDANI

SCCS/AGM/MIKOPO/2017

TAREHE: 24 DISEMBA 2017

**KUTOKA: BODI YA WAKURUGENZI
POSTA NA SIMU
SACCOS LTD.**

**KWENDA: WANACHAMA
MATAWI YOTE**

YAH: AZIMIO LA BARAZA KUHUSU AINA YA MIKOPO

Tafadhali husika na somo tajwa hapo juu.

Katika Mkutano wa Kawaida wa Baraza la Wawakili uliofanyika tarehe 17 Disemba 2017, katika Ukumbi wa **NSSF MAFAO HOUSE ILALA DAR ES SALAAM** Taarifa ya Kamati ya Mikopo ilijadiliwa. Baada ya Majadiliano ya kina Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi waliazimia aina ya Mikopo kama ifuatavyo :-

(a) Mkopo wa Maendeleo (Planned Loan)

Mkopo wa Maendeleo utatolewa mara mbili (2) ya Akiba za Mwanachama kwa Marejesho yasiyozidi miezi Thelathini na Sita (36) na riba ya asilimia mbili (2%) kwa mwezi (Reducing balances)

(b) Mkopo ya Elimu na Mkopo midogo

Mkopo wa Elimu na Mkopo Midogo imeunganishwa na mkopo wa Dharula. Hivyo mkopo wa Dharura utatolewa kuanzia Tshs Moja hadi Tshs Milioni Tatu (Tshs 1 – 3M) kwa marejesho yasiyozidi miezi sita (6) na riba ya asilimia mbili (2%) (reducing balances).

Utekelezaji wa aina hii ya mikopo utaanza kutolewa kuanzia tarehe 01 Januari, 2018.

Tunatanguliza shukrani za dhati kwa ushirikiano kwa utekelezaji wa Azimio hili

“Pamoja na Salamu za Ushirika”

**J.N. MISSELYA
KATIBU WA BODI**